Toleo 53

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## MWALIKO MKUU ZAIDI—WENGI WAMEITWA

*(Mfano ambao ulitolewa na Kristo—kama inavyonakiliwa katika Mathayo 22:1-14)*

Yesu alitoa mfano kuhusu sherehe ya harusi ya kifalme, akionyesha umuhimu wa mwaliko wa wokovu ambao umetolewa kwa watu wote.

Ufalme wa Mungu unafananishwa na mfalme ambaye alifanya chakula cha jioni kwa ajili ya sherehe ya ndoa ya mwana wake. Mfalme huyo akatuma watumishi wake kuwaita watu walioalikwa kuja kwenye harusi, lakini hawakufika. Ndipo akawatuma watumishi wengine wakiwa na habari kemkem kuhusu chakula hicho cha jioni ambacho tayari kilikuwa kimeandaliwa "Njooni kwa harusi, kila kitu kiko tayari!"

Wengi walioalikwa walijibu wakiwa na mwelekeo wa kutojali au madharau, huku wakiendelea na shughuli zao—wengine wakienda kufanya kazi mashambani mwao, na wengine wakiendelea na biashara zao. Lakini wengine, wakiwa na hasira dhidi ya mfalme huyo, walifanyia watumishi hao vibaya na mwishowe kuwaua. Mfalme akasikia habari hii ya kuvunjiwa heshima na kufanyiwa mambo yasiyo ya haki; ndipo akatuma wanajeshi wake kuwaua wauaji hao na kuharibu miji yao.

Mfalme akawaambia watumishi wake, "Arusi i tayari, lakini wale walioalikwa hawakustahili.Basi enendeni hata kwenye njia panda muwaite wote waje kwenye sherehe." Watumishi hao wakaenda na kufanya kama vile walivyoamuriwa na mfalme, wakawaalika watu wote—wazuri na wabaya—ili waweze kufika kwenye sherehe ya arusi. Punde si punde harusi ikawa imejaa wageni.

Ndipo mfalme akaja kuwaona wageni, na akamuona mtu mmoja ambaye hakuwa amevaa vazi la harusi. "Rafiki, uliingiaje humu nawe huna vazi la arusi?" mfalme akamuuliza. Bwana huyo hakuwa na la kusema. Ndipo mfalme akaamuru watumishe wake wamfunge mtu huyo miguu na mikono na kumtupa nje kwenye giza, ambako kungekuwa na mateso mengi.

Yesu anatamatisha mfano huu kwa kusema kwamba, "Waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache."

Mfano huu unatupatia msingi wa ukweli mkuu wa mafundisho ya kidini. Mwaliko mkuu kabisa ambao umewahi kutolewa ni kwamba watu waokolewe kutokana na dhambi zao, na kuweza kupokea baraka za ufalme wa Mungu. Mwaliko huo kwanza ulitolewa kwa Wayahudi, lakini kama taifa wao walimkataa Yesu Kristo na kudharau mweke huo wa kufanya toba na kufurahia wema wa Mungu. Ndiposa habari njema ya wokovu ikasambazwa na kuwafikia watu wa Mataifa. Mwaliko huu wa Mungu kuhusu wokovu ulitolewa kwa watu wa kila familia, taifa, tabaka, na lugha. "Njooni muokolewe. Tubuni na kuunganishwa na Kristo, ili muweze kuingia kwenye furaha ya Bwana."

Lakini watu wengi huwa na nia mbili katika witikio wao kwa mwaliko wa harusi—wengi wakiupuuza kwa njia ambayo si dhahiri. Wao huwa wakishughulika sana na shughuli za maisha ya sasa, na kukosa kuwa makini kwa utumishi wa Mungu. Aidha wanatilia pesa maanani, raha, elimu yao, kazi, au kujifurahisha, na kwa hivyo wanakosa kuitika mwaliko wa injili. Wengine nao huleta pingamizi na wanakuwa waasi wanaopigana na mambo ya Mungu.




"Mwaliko mkuu kabisa ambao umewahi kutolewa ni kwamba watu waokolewa kutokana na dhambi zao, na kuweza kupokea baraka za ufalme wa Mungu.."


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Tahariri | Mwongozo wa Kujifunza Biblia: Kuteuliwa na Uamuzi Ulio Huru | Kuteuliwa kwa Njia ya Neema | Maswali na Majibu | Endelea Kuwaalika—Mungu Angali Anaitana |
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

Ni muhimu kutambua kwamba mwaliko wa injili umetolewa kwa watu WOTE—hakuna mtu amewekwa nje ya wito huo. Mfalme alitaka watu wote kuja kwa karamu ya harusi, kama ambavyo Mungu anataka watu wote waokolewe hadi leo. Yeye anataka uje na ufurahie karamu yake ambayo ni murwa, katika maisha haya na katika maisha yajayo.

Kama ilivyo kwa harusi zote kila mtu anatarajiwa kuja kwa harusi na mavazi yanayofaa. Katika nyakati za Yesu, kwa kawaida wageni walipewa mavazi ya arusi na bwana-arusi; haikuwa kwamba wajinunulie mavazi hayo. Mungu ametoa mahitaji ya wale WOTE ambao watakubali mwaliko wake—amewatolea kila mmoja wao mavazi ya utakatifu. Utakatifu wetu wa kibinafsi haukubaliki katika harusi hiyo. Mavazi pekee ambayo yanakubalika ni wokovu ambao ni Mungu tu anaweza kumpatia mtu. Lakini ili mtu apokee wokovu yeye binafsi lazima ajitoe kwa mwaliko huo wa wokovu ulio kwa ajili ya watu wote.



"Utakatifu wetu wa kibinafsi haukubaliki katika harusi hiyo. Mavazi pekee ambayo yanakubalika ni wokovu ambao ni Mungu tu anaweza kumpatia mtu.."

Haitoshi mtu kufika kwa ibada za kanisa au kushirikiana na wageni. Lazima tuvalishwe vazi la wokovu. Hii ndio sababu yule bwana katika mfano huu hakuwa na cha kusema—kwa sababu hakuwa na kisingizio. Alikuwa amepewa vazi la kuvaa lakini akakataa kulivaa. Kukataa huko kulimletea hasara kubwa: akatenganishwa na uwepo wa mfalme milele na kutupwa mahali pa mateso.

Mungu hamlazimishi mtu yeyote kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wake; ila watu WOTE wamealikwa. Baadhi ya watu hupuuza mwaliko huo, ilhali wengine hukawia kuukubali wito huo. Wengine huitika lakini wanadumisha mafundisho yao ya kidini na njia zao wenyewe, na wanakataa kukubali njia za Mungu za utakatifu. Kama ilivyo katika mfano huu, watu wote wameitwa, lakini sio wote wamechaguliwa kufurahia baraka za Mungu, kwa sababu wao hawako tayari kufuata matakwa yaliyowekwa.

Wale ambao wamechaguliwa—walioteuliwa na Mungu na kubarikiwa katika maisha haya na ya milele—ni wale ambao watakubali wito wake na kuvaa mavazi ambayo yametolewa kwa ajili ya harusi. Mwaliko mkuu umetolewa kwetu sote, lakini ni lazima tukubali wito huo na kuvalishwa mavazi ya wokovu. Kwa maana kama Yesu alivyosema, "Waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache." Mungu hamkatazi mtu yeyote nafasi ya kupata wokovu. Kipawa hiki cha Mungu kimetolewa kwa watu wote kwa neema yake bila malipo, lakini ni lazima kila mtu aamue kukipokea.

**Je, rafiki yangu, wewe umeitikia mwaliko huo mkuu? Je, siku hiyo kuu utasimama kama umevaa haki ya Yesu? Basi usichelewe—wokovu unakusubiri.**

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe.* – Yohana 7:37

Yesu alitoa mwaliko wazi kwa watu wote ambao wana kiu cha ndani—wale ambao wana shauku ya kupata kitu ambacho kina chake ni cha ndani zaidi, kitu bora zaidi, na cha milele. Mimi nina shukrani sana kwamba tumealikwa ili tupate wokovu. Neema ya Mungu imesambazwa kwa watu wote, na shauku yake ni kwamba kila mtu aikubali kwa imani.

Somo la robo hii ya mwaka ni "Kuteuliwa na Uamuzi Ulio Huru." Maswali ya (mafundisho ya) kidini ambayo yamezunguka swala hili yamejadiliwa kwa karne nyingi. Kulingana na thiolojia ya Kalvini—ambayo msingi wake ni mafundisho kama yale ya watu kuteuliwa bila vikwazo, utakaso ambao una mipaka, neema ambayo haiwezi kukataliwa, na kudumishwa kwa wateule—ni mafundisho ambayo yanaharibu  ujumbe mzuri wa wokovu. Mafundisho haya yanapinga ukweli wa biblia kwamba shauku la Mungu ni kwamba watu wote waokolewe kutokana na dhambi zao.

Badala ya mimi kutumia wakati wangu kupinga kila dhana ambayo sio sahihi, toleo hili linatilia mkazo ukweli halisi—ambao umeelezwa kinagaubaga katika Maandiko yote—kwamba wokovu umetolewa kwa watu wote na unahitaji kupokelewa bila malipo. Njia bora zaidi ya kukabiliana na mafundisho ya uwongo ni kuweka ukweli wazi. Wakati tunajifunza Neno la Mungu na kulifasiri kwa njia sahihi, hapo ndipo tunapata uwezo wa kutambua na kupinga mambo ambayo sio ya ukweli. Maandiko yanayonukuliwa kutoka hapa na pale yanaweza kuonekana kama kwamba yanaunga mkono mafundisho fulani ya kidini, lakini ni lazima Maandiko yafasiriwe katika muktadha wake, na kwa njia ambayo inakubaliana na ujumbe wote wa injili. Msingi wa mafundisho ya Agano Jipya ni kwamba wokovu umetolewa kwa watu wote—na wala sio kwa watu wachache ambao walichaguliwa tangu asili. Mungu amempatia kila mtu uhuru wa kuchagua kama atapokea au hatapokea neema yake.

Maandiko mengi ambayo yanataja swala la kuteuliwa hasa huzungumzia kubadilishwa kwa agano ambalo Mungu alifanya na wana wa Israeli, hadi ikafika kwa kuitwa kwa kanisa la Agano Jipya. Yanaposomwa kwenye muktadha wake, inakuwa dhahiri kwamba maandiko hayo hayazungumzii wokovu wa kibinafsi wa nafsi za wanadamu, bali kuhusu mpango kamili wa ukombozi kupitia kwa Kristo.

Je, kudai kwamba Kristo hakufa kwa ajili ya wote wote si ni ujumbe wenye huzuni na usio wa kweli—kusema kwamba damu ya Yesu inafaa tu kwa watu wachache ambao walichaguliwa hapo awali. Mungu asifiwe kwa sababu neema yake inakufikia wewe na mimi! Katika upendo wake ambao msingi wake ni utawala wake  mkuu, Mungu ametupatia uhuru wa kukubali au kukataa kipawa cha wokovu.

Ingawa somo hili haliwezi kufundishwa kwa mapana na marefu katika toleo kama hili moja, tunaamini kwamba hapa tumeweka msingi mzuri kwa swala hili. Hebu basi Roho wa Mungu akuongoze hadi uweze kufikia kuelewa kwa kina na pia uweze kuimarishwa katika ukweli wa Neno lake.

Michael W. Smith

Julai, 2025

*Tutembelee*

*www.thegospeltruth.org*

*ili kujiandikisha na*

*kupata jarida*

*za mbele.*

**Toleo la Ukweli wa Injili Linalofanana na Hili: Toleo la 28:**

**Usalama wa Milele**




## Ikiwa Mungu tayari anajua mambo yote,

### hii ni kusema kwamba hatuwezi kufanya uchaguzi halali?

**La.** Ingawa Mungu anajua mambo yote na Yeye ni mtawala mkuu, Yeye pia alituumba  na uwezo wa kuchagua tutakayofanya. Uwezo wake wa kujua mambo yote mapema haumaanisha kwamba Yeye ndiye chanzo cha maamuzi yetu. Wakati mambo yatakayokuja yalitabiriwa kwa uwezo wa Mungu wa kujua mambo yote mapema—yaani uwezo wake ulio kamili wa kujua mambo yatakayotendeka—ufahamu huo wake sio ambao unawafanya wanadamu kufanya wanayofanya, bali kwamba Yeye aliwajulisha wanadamu mambo hayo mapema kabla hayajatendeka.

Unabii unaopatikana kwenye Maandiko—kama ule ulio kwenye vitabu vya Danieli na Ufunuo—ulifunuliwa sio kwa kusudi la kubatili maamuzi ya wanadamu, bali lengo lake lilikuwa ni kudhihirisha kwamba Mungu anajua mwisho wa mambo kuanzia mwanzo wake. **Uwezo wa Mungu wa kujua mambo awali unatilia mkazo utawala wake mkuu, pasipo kuzorotesha uwezo wa wanadamu wa kufanya maamuzi yao wenyewe.**



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Kuteuliwa na Uamuzi Ulio Huru

### Utawala Mkuu, Neema, Uchaguzi, Wokovu

**Masomo ya Maandiko:** *Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako.*—Kumbukumbu 30:19

**Kutoa Maana:** **Kuteuliwa:** Tendo la Mungu la kuchagua au kuteua. Kuteuliwa huku kunaambatanishwa na neema ya Mungu na uwezo wake wa kujua mambo hapo awali, sio kwa mapendeleo au kulazimishwa.
**Uchaguzi Ulio Huru:** Uwezo ambao Mungu amewapatia wanadamu wa kufanya maamuzi. Kwenye muktadha wa wokovu jambo hili linahusishwa na uwezo wa kukubali wito wake Mungu—aidha kwa kuikubali au kuikataa neema ambayo ametoa kwetu.

**Muhtasari:** Neema ambayo inatokana na utawala mkuu wa Mungu hufanya kazi kwa kuandamana na jukumu la mwanadamu na uhuru wake wa kuamua. Mungu alipanga mpango wake wa kiasili wa wokovu kupitia kifo cha Yesu Kristo, mpango ambao ulikusudiwa kuwafikiwa watu wote. Yeye anatuita na kutualika ili tuukubali.

---

#### I. Utawala Mkuu wa Mungu

A. Isaya 46:9-10 Shauri la Mungu litasimama.
B. Danieli 4:45 Mungu hufanya kama atakavyo.

#### II. Wito wa Wokovu kwa Watu Wote

A. Yohana 3:16-17 Mungu aliupenda ulimwengu.
B. 1 Timotheo 2:4 Mungu hutaka watu wote waokolewe.
C. 2 Petro 3:9 Mungu hapendi mtu yeyote apotee.
D. Mathayo 11:28 Njoni kwangu.
E. Ufunuo 22:17 Yeye atakaye aje.

#### III. Kristo Alikufa kwa Ajili ya Watu Wote

A. 1 Timotheo 2:6 Alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote.
B. 1 Yohana 2:2 Yeye ndiye kipatanishi cha dhambi za ulimwengu wote.
C. Waebrania 2:9 Alionja mauti kwa ajili ya kila mtu.
D. 2 Wakorintho 5:15 Alikufa kwa ajili ya wote.
E. Yohana 1:29 Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.

#### IV. Tunapata Wokovu kwa Njia ya Neema Kupitia Imani

A. Waefeso 2:8-9 Mmeokolewa kwa neema . . . hiyo haikutokana na nafsi zenu.
B. Tito 2:11-12 Neema imefunuliwa kwa watu wote.
C. Warumi 3:24 Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake.
D. Matendo 15:11 Tutaokoka kwa neema ya Yesu.

#### V. Uamuzi Ulio Huru na Uchaguzi wa Mtu Binafsi

A. Kumbukumbu 30:19 Chagua uzima ili uwe hai.
B. Yoshua 24:15 Chagueni mtakayemtumikia.
C. Waebrania 3:15 Msifanye migumu mioyo yenu.
D. Warumi 6:16 Kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kumtii.
E. 2 Petro 1:10 Kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu.

#### VI. Kupokea au Kupinga Neema

A. Ufunuo 3:20 Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango.
B. 2 Wakorintho 6:1 Msiipokee neema ya Mungu bure.
C. Mathayo 23:37 Nimetaka . . . lakini hamkutaka.
D. Matendo 7:51 Mnampinga Roho Mtakatifu.
E. Waebrania 7:51 Wokovu kwa watu wote wanaomtii.
F. Matendo 24:25 Feliki alijaa hofu lakini akajicheleweshа.

#### VII. Kuteuliwa kwa Neema na Kuchaguliwa Tangu Awali

A. 2 Timotheo 1:9 Wokovu ulipangwa tangu milele.
B. Waefeso 1:4-7 Alituchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.
C. Waefeso 1:10-11 Kuchaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake.
D. Warumi 8:28-30 Aliowajua tangu asili aliwachagua tangu asili, akawaita; akawahesabia haki.
E. Matendo 4:12 Hakuna wokovu katika mwingine awaye yote.
F. 2 Wathesalonike 2:213 Amewachagua tangu mwanzo.
G. 1 Petro 1:2 Wateule kulingana na kama vile Mungu Baba alitangulia kuwajua.
H. Yohana 1:11-13 Sio kwa mapenzi ya mtu.
I. Warumi 11:5-7 Mabaki walichaguliwa kwa neema.

#### Tamati

*Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure.*—Ufunuo 22:17

# Kuteuliwa kwa Njia ya Neema

## UTAWALA MKUU WA MUNGU NA WITIKIO WA UCHAGUZI HALISI



Mungu anawaita watu wote ili waokoke, lakini sio wote huitika. Je, utawala mkuu wa kiungu na uchaguzi wa mwanadamu huenda sambamba kwa njia gani? Kuteuliwa kwa njia ya neema ni dhihirisho la utawala mkuu wa Mungu—ambao unamwita kila mwanadamu kuitika wito wake. Chaguo ni letu.

"Hata hivyo, ingawa wanadamu wanaweza kutenda nje ya mapenzi yake Mungu, uhuru huo wa kuchagua uko ndani ya mwanadamu kupitia kwa mpango wake Mungu."

### Mpango wa Wokovu Ambao Unatokana na Utawala Wake Mungu

Mungu ni mtawala mkuu juu ya vyote. Hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kwenda kinyume na mapenzi yake, kusudi, na mipango yake. Kama ambavyo nabii Isaya alitangaza, "Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote" (Isaya 46:10). Mungu huongoza mambo yote kulingana na hekima na kusudi lake la kiungu. Kama alivyotangaza Danieli, "Naye hufanya kama atakavyo . . . wala hapana awezaye kuuzuia mkono wake" (Danieli 4:35). Jambo hili linajumuisha hata mpango wake wa wokovu. Mungu alikusudia kuwakomboa wanadamu kabla ya ulimwengu kuwekewa misingi yake. Wokovu haukuwa jambo lililotokea kwa bahati tu—bali ulikuwa ni mpango uliolingana na kusudi lake Mungu, lengo lake likiwa ni kuwafikia watu wote.

### Mwaliko kwa Watu Wote

Injili ni wito unaotolewa kwa watu wote. Mungu anapenda ulimwengu wote na ndiposa akafanya wokovu upatikane na "kila mtu amwaminiye" (Yohana 3:16). Mungu "hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli" (1 Timotheo 2:4). Petro alitangaza mapenzi ya Mungu kwamba: Bwana "hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9). Mwaliko wa Roho umesambazwa kwa watu wote: "Yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure" (Ufunuo 22:17).

Yohana Mbatizaji akatangaza, "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29). Wokovu haujatengwa kwa ajili ya watu wachache tu walioteuliwa. Yesu "alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote" (1 Timotheo 2:6) ili kuwa kafara ya upatanisho wa dhambi "kwa dhambi za ulimwengu wote" (1 Yohana 2:2). Yeye "alikufa kwa ajili ya wote" (2 Wakorintho 5:15) na alionja mauti "kwa ajili ya kila mtu" (Waebrania 2:9). Hakuna mtu aliyewekwa kando ya mpango huo!

### Wokovu Kupitia Neema

Ingawa wokovu umetolewa bila malipo, wokovu huo haumfikii mtu kwa njia ya moja kwa moja, na pia haukubaliwi na watu wote. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani . . . si kwa matendo" (Waefeso 2:8-9). Wokovu hautolewi kwa misingi ya cheo cha mtu, kazi zake, ukoo wake, kustahilihi kwake, bali ni kwa neema—kwa wema wa Mungu ambao hakuna mtu anayeweza kuustahili. "Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu" (Warumi 3:24). Ukombozi hupatikana tu "kwa neema ya Bwana Yesu" (Matendo 15:11). Ingawa wokovu huu haukubaliwi na watu wote, umetolewa kwa watu wote. "Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa" (Tito 2:11-12).

### Nguvu za Uchaguzi Huru

Mapenzi ya Mungu ni kwamba watu wote waokoke, na Kristo alikufa ili kutimiza kusudi hili la kiungu. Lakini pia sehemu ya utawala wake mkuu ilikuwa kwamba mwanadamu awe kiumbe chenye uchaguzi huru—maanake uwezo wa kuchagua cha kufanya. Mungu alipowaumba wanadamu kama viumbe wenye uchaguzi huru, hili ni jambo ambalo lililingana na utawala wake mkuu. Hata hivyo, ingawa wanadamu wanaweza kutenda nje ya mapenzi yake Mungu, uhuru huo wa kuchagua uko ndani ya mwanadamu kupitia kwa mpango wake Mungu.

Maandiko yanasema kwamba wanadamu wana jukumu la kufanya maamuzi yao. "Nimekuwekea mbele yako uzima na mauti... basi chagua uzima" (Kutoka 30:19). Kwa njia hiyo hiyo, Yoshua aliwapa watu changamoto kwamba: "chagueni hivi leo mtakayemtumikia" (Yoshua 24:15). Bila uwezo wa kuchagua hakuwezi kuwa na ibada au upendo wa kweli.

Waebrania 3:15 nayo inatuhimiza tufanye witikio wa kibinafsi: "Leo, kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu." Kama viumbe vyenye uchaguzi huru tuna uwezo wa kutii au kumkataa Mungu. Ndiposa Paulo aliandika na kusema, "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake" (Warumi 6:16). Kila mtu anawajibika kwa ajili ya hatma ya nafsi yake. Ndiposa Paulo anatoa wito kwamba "Jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu" (2 Petro 1:10). Kama hakungekuwa na uchaguzi huru basi wito wa aina hio haungehitajika.

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)*

## Kupokea au Kupinga Neema

Uamuzi wa mwanadamu ambao uko nje ya kusudi la Mungu kamwe hauzoroteshi utawala mkuu wa Mungu—bali unadhihirisha utawala huo. Uwezo wa mwanadamu wa kuchagua unatokana na uwezo wa Mungu, lakini jukumu la kuchagua huwa ni la yule anayehusika. Kulingana na mpango wa utawala wa Mungu, ni jukumu la kila mtu binafsi kukubali au kukataa neema ya wokovu. Kristo amesimama nje ya kila moyo wa mwanadamu akibisha: "Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake" (Ufunuo 3:20). Wokovu lazima upokelewe. Kila mtu lazima afanye uchaguzi wake: "Msiipokee neema ya Mungu bure" (2 Wakorintho 6:1).



> "Kuteuliwa kwa neema ni jambo ambalo linaunganisha utawala mkuu wa Mungu na witikio wa wanadamu—wale ambao wanaamini wamechaguliwa, sio kwa lazima, bali kwa neema."

Yesu alitazama mji wa Yerusalemu kwa majonzi na kusema: "Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako . . . lakini hamkutaka" (Mathayo 23:37). Bwana alitaka kuwa Mwokozi wao, lakini wao wakamkataa. Stefano naye akawakemea viongozi wa kidini huku akisema, "Siku zote mnampinga Roho Mtakatifu" (Matendo 7:51). Feliki naye alikuwa ameshawishika na kuvutiwa kufanya toba, lakini akaamua kuipinga (Matendo 24:25). Yesu naye "akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii" (Waebrania 5:9). Mungu humwita kila mtu, lakini kila mtu lazima akubali au kukataa wokovu.

## Kuteuliwa kwa Njia ya Neema

Ingawa wokovu umetolewa kwa watu wote na kila mtu lazima afanye uchaguzi wa kuitikia, Biblia pia inasena kuhusu uteuzi wa Mungu—ambao ni uchaguzi wake unaotokana na utawala wake mkuu kwa njia ya neema. Hebu zingatia jinsi mwaliko wa Mungu na witikio wa mwanadamu hufanya kazi ndani ya kusudi lake la milele na uelewaji wake wa kiasili wa hapo awali. Wokovu haukuwa kitu kilichotokana na wazo la baadaye—bali wokovu ni jambo la kiungu lililopangwa na Mungu kabla ya wakati kuanza. Ukombozi wa Mungu ulipangwa kabla ya wakati kuanza. Kama ambavyo Paulo aliandika, Mungu "alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele" (2 Timotheo 1:9). Kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu Mungu alianzisha mpango wa neema kupitia Yesu Kristo. Lakini ingawa mpango huo ulianzishwa kutokana na utawala wake mkuu, mpango wenyewe ulihusisha njia ambayo watu binafsi wangeweza kupokea wokovu huo—kupitia imani na kutii.

## Kuchaguliwa Tangu Awali

Waefeso 1:4-5 inasema, "kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo." Wale waliochaguliwa na walioteuliwa ni wale ambao watakuja kwa Kristo kwa njia ya imani. Mstari wa 11 unaongezea kusema, "Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake." Mungu alipanga tangu awali mpango huo ambao waumini wangepokea urithi—sio kwamba Yeye aliandaa orodha ya watu binafsi, bali kwamba tangu awali alipanga kusudi lake kwa watu wote ambao wataitikia wito wa Kristo.

Wokovu haukutolewa kwa ajili ya kikundi kimoja tu. Mtume Paulo alifundisha katika maandishi yake yote kwamba mpango wa Mungu uliwahusisha Wayahudi na pia watu wa mataifa. Warumi 8:28-30 inafundisha kwamba wale ambao Mungu alijua tangu awali pia aliwachagua tangu awali. Wito wa injili ulipangwa kabla ya kuja kwa Kristo, na kusambazwa kwa watu wote. Njia ya wokovu tayari imewekwa: "Kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12). Mungu hakuchagua tangu awali wale ambao wangeamini, bali kwamba wale watakaoamini wataokolewa.

Wathesalonike wa pili 2:13 inasema, "Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli." Kuteuliwa na Mungu—kuchaguliwa na Yeye—silo jambo lililo kando na witikio wa mwanadamu. Wale ambao wamechanguliwa ni wale ambao wataamini. Petro anathibitisha hili katika 1 Petro 1:2 kwa kuwaita watakatifu "wateule . . .(kama) vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua." Uamuzi wa Mungu wa kuwapatia wokovu wote watakaoamnini—Wayahudi na watu wa mataifa—ni ufunuo wa fumbo hilo la kuteuliwa na kuchaguliwa kwa tangu awali. Wanadamu sasa hawafanyiki wana wa Mungu kwa njia ya ukoo na utaifa, bali ni kwa kulingana na uchaguzi kwa njia ya neema kupitia imani.

Ukweli huo unakaririwa tena katika Yohana 1:11-13: "Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu." Ingawa Wayahudi kama taifa walimkataa Kristo, wote ambao walimpokea walifanyika kuwa wana wa Mungu, sio kwa haki ya kuzaliwa au mapenzi ya mwanadamu, bali kupitia imani katika Kristo.

## Chaguo ni Lako

Mtume Paulo alitamatisha swala hili katika Warumi 11:5: "Basi ni vivi hivi wakati huu wa sasa, yako mabaki waliochaguliwa kwa neema." Kuchaguliwa kwa neema ni jambo linalozungumzia wale ambao wataamini kulingana na mpango wa Mungu. Kuteuliwa sio tangazo ambalo halina msingi dhabiti, bali kwamba ni mpango wa neema ya Mungu kwa ajili ya watu wote ambao wataitikia injili. Wito ni kwa watu wote, lakini wale ambao wanaitikia ndio walioteuliwa.

Kuteuliwa kwa njia ya neema ni jambo ambalo huunganisha utawala mkuu wa Mungu na witikio wa mwanadamu—wale ambao wanaamini wamechaguliwa, sio kwa kulazimishwa, bali kwa neema. Mpango tayari umeandaliwa, dhabihu tayari ishatolewa, wokovu nao umetolewa—sasa chaguo ni lako! ■

# Maswali na Majibu

## Je, ikiwa sifa za maumbile za mwanadamu ni potovu kabisa, inawezekanaje mtu yeyote kuamua kumtafuta Mungu?

Nabii Yeremia alielezea hali ya kuanguka ya wanadamu: "Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?" (Yeremia 17:9). Paulo naye anasema maneno kama hayo katika Warumi 3:10: "Hakuna mwenye haki hata mmoja." Mstari wa 12 nao unaongezea kusema, "Hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja" Kabla ya kupokea wokovu kila mwanadamu huwa katika hali ya upotovu. Hiyo si kumaanisha kwamba wanadamu hawawezi kufanya jambo lolote nzuri, bali ni kwamba hakuna mwanadamu yeyote mwenye haki machoni pa Mungu—sisi sote tunahitaji wokovu.

Katika Warumi 3 Paulo anazungumza kuhusu Wayahudi, akionyesha kwamba hawakuwa katika hali bora zaidi kuliko watu wa Mataifa, kwa sababu wao wote walikuwa katika hali moja ya dhambi. Bila kupata wokovu watu wote hupungukiwa na utakatifu wa Mungu. Paulo anasema katika mstari wa 11, "Hakuna amtafutaye Mungu."

Jambo hili linazua swali hilo tena: Je, inawezekanaje mtu mwenye hali ya upotovu kumtafuta Mungu? Yesu alitoa jawabu kuhusu jambo hilo kwa njia ya moja kwa moja: "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka" (Yohana 6:44). Mvuto wa Roho Mtakatifu unahitajika ili kumleta mtu ambaye hajaokoka kufikia mahali pa kufanya maamuzi. Hakuna mtu anayemtafuta Mungu ila kwa neema yake. Lakini habari njema ni kwamba neema hiyo inayotuvutia huwafikia watu wote.

Yesu alisema kwamba Roho Mtakatifu akija "atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu" (Yohana 16:8).

Tena akatangaza kwamba, "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu" (Yohana 12:32). Yohana 1:9 inasema Yesu ni "Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu." Neema hii ya kuhakiki na kuwavuta watu haijatolewa kwa watu ambao walichaguliwa hapo awali—ila imesambazwa kwa watu wote, hata kwa wenye dhambi wakuu. Yesu alikuja "kutafuta na kuokoa kile kilichopotea" (Luka 19:10).

Mungu ndiye mwanzilishi, na ndiye huwaita watu, anawahakiki dhambi zao, anawapa mwangaza, na anawavutia kwake. Lakini mwenye dhambi ana jukumu la kuitikia wito huo kwa imani au kuukataa. Hata ingawa hakuna mtu anayemtafuta Mungu kwa nia yake mwenyewe, kila mtu hupata mvuto huo, na ndiposa jukumu la kuitikia ni la kila mwanadamu. Hata shauku iliyo ndogo sana ndani yetu kumwelekea Mungu haitokani nasi wenyewe—bali ni dhihirisho la neema yake inayotuvutia.

## Ikiwa Yesu alisema "Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi," hii ni kumaanisha kwamba hatuna uchaguzi wa kufanya kuhusiana na swala la wokovu?

La. Wokovu umetolewa bila malipo, lakini hakuna mtu anayelazimishwa kuupokea. "Yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure" (Ufunuo 22:17).

Swali linaulizwa hapa linatokana na Yohana 15:16 "Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda." Mizizi ya neno hili "niliyewachagua" inatoka mahali moja na neno lingine "niliyewateua." Muktadha wa maandiko ni jambo muhimu sana tunapojifunza Neno lake Mungu.

Katika maandiko yanayonukuliwa hapa Yesu alikuwa akiwalenga wanafunzi wake. Kristo ndiye aliyewaita na kuwaweka wakfu ili waende wakahubiri injili. Wito wao na vipawa vyao vya kiroho havikutokana na wao wenyewe—ni mambo yaliyotokana na Mungu. Ingawa wito wa wokovu umetolewa kwa watu wote, mstari wenyewe unazungumzia wito wa wanafunzi katika utumishi wao na huduma yao—na maneno hayo kamwe hayapingi uwezo wa wanadamu wa kufanya maamuzi ya kupokea wokovu.

## Je, Warumi 9 inafundisha kwamba Mungu huwachagua wale wataokolewa na wale ambao hawataokolewa?

**La.** Warumi sura ya 9 inatilia mkazo haki yake Mungu ambayo inatokana na utawala wake mkuu ya kumbariki yeyote anayetaka na haki yake ya kutimiza mpango wake wa wokovu. Sura hii haifundishi kuhusu wokovu ambao hauna msingi dhabiti. Wakati Mungu anasema, "Nimempenda Yakobo, bali Esau nimemchukia" (mstari 13) hakuwa akizungumzia Yakobo na Esau kama watu binafsi, ila alikuwa akinena kuhusu uzao wao. Alikuwa akizungumza kuhusu mataifa na majukumu yao katika mipango wake—sio kuhusu wokovu wa watu binafsi. Kama vile Mungu kupitia utawala wake mkuu aliamua kuwabariki wana wa Yakobo juu ya mataifa yote, ndivyo hivyo alivyo na haki ya kufungua mpango wake wa wokovu kwa watu wa Mataifa. Basi walioteuliwa hawategemei uzao wao wa Kiyahudi, bali ni kulingana na kuzaliwa kwao kiroho.

"Nitamhurumia yeye nimhurumiaye" (mstari 15) ni mstari unaotangaza kwamba rehema ni za Mungu na ni Yeye huzitoa. Lakini kuna maandiko mengine yanayoonyesha kwamba Yeye hutoa rehema na wokovu kwa watu wote. Mtume Paulo aliendelea kuandika na kusema, "si katika uwezo wa yule atakaye . . ." (mstari wa 16), hili ni jambo linalotilia mkazo kwamba wokovu haupatikani kutokana na bidii za kibinadamu—bali ni kwa kupitia neema. Basi Warumi 9 inasisitiza haki ya Mungu ya kutoa rehema zake kulingana na matakwa yake—matakwa ambayo inawaalika watu wote kumwitikia kwa imani.

Lakini andiko hili lina onyo ndani yake: mtu akiendelea kukataa mienendo ya Mungu, na Mungu anafikia kumwondolea uhakiki wa Roho wake, basi moyo wa mtu kama huyo utakuwa ngumu.

JE, WAJUA?

Ukalvini na Uarimini ni mafundisho yanayosimamia misimamo miwili mikuu kuhusiana na wokovu. Ukalvini, ambao chimbuko lake ni mafundisho ya Yohana Kalvini (1509-1564), ni mafundisho ambayo yanatilia mkazo utawala mkuu wa Mungu unaounganisha swala la kuchaguliwa tangu awali, ambalo ni imani kwamba Mungu huwateua watu ili waweze kupata uzima wa milele. Lakini Uarimini, ambao msingi wake ni mafunzo ya Yakobo Arminius (1560-1609), ni mafundisho yanayotilia umuhimu uchaguzi huru wa wanadamu, na kusema kwamba watu wanaweza kukubali au kukataa neema yake Mungu. Mitazamo hii inatofautiana kwa maswala ya kuteuliwa, neema, na kudumishwa kwa wokovu—na kutokana na mitazamo hii miwili, kumekuwa na mijadala kuihusu kwa karne ya miaka.

Lakini ni baraka kuu zaidi sisi kusimama katika mwaliko rahisi na wazi ambao Kristo aliufanya: "Njoni kwangu . . . nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# ENDELEA KUWAALIKA—MUNGU ANGALI ANAITANA

*Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa*—Luka 14:23



Mtu anaweza kufa moyo ikiwa atashiriki injili lakini ikataliwe, akutane na pingamizi, au apatane na mwelekeo wa kutojali. Lakini Yesu alipitia haya yote, na hata nasi pia tutakutana nayo. Walakini, Mungu angali anaitana, na mwaliko wake ungali hujapitwa na wakati. Mlango wa neema ungali u-wazi. Jukumu letu sio kuamua ni nani ataitikia, bali ni la kuenenza mwaliko huo kwa uaminifu.

Hata katika huduma ya Paulo kuna wale waliomdhihaki, wengine wakachelewa kufanya uamuzi, ilhali wengine waliamini. Matokeo yalikuwa tofauti tofauti, lakini mwito wake haukubadilika. Basi wewe endelea kuhubiri. Endelea kupenda. Endelea kutumika. Endelea kufanya mwaliko.

Kungali kuna mioyo itakayosema "ndio." Kuna wana wapotevu ambao bado watarudi nyumbani. Kungali kuna nafsi za watu ambazo zina njaa ya kujua ukweli, ambazo zinatafuta tumaini, na ambazo ziko tayari kupokea vazi la haki. Huenda hawatakuja wakiwa halaiki ya watu, lakini hata mwenye dhambi mmoja akiokoka kunakuwa na furaha kuu Mbinguni. Mbengu tunayopanda haizai matunda mara moja, na matokeo yake sio jukumu letu. Wito wetu ni kupanda tu mbengu nzuri za injili.

Watu wanapoitikia wito wetu haitakuwa ni kwa sababu ya ufasaha wetu wa kusema, mikakati yetu, au hekima yetu—itakuwa ni kwa sababu ya rehema na neema yake Mungu. Jambo hili linahitaji kukupatia nguvu za kuwaita watu wote bila woga. Hatuhitaji kusitasita kuwaambia watu kumhusu Yesu, kwa sababu hatuwapatii kitu kilicho dhaifu au kisicho na uhakika. Tunatangaza kipawa kikuu zaidi katika ulimwengu huu: wokovu.

Ingawa wakati wa hukumu umewadia, hukumu hiyo bado haijafika. Basi wakati ambapo kungali na uhai, Mungu angali anaitana. Na kwa sababu angali anaitana, sisi nasi tunahitaji kuendelea kuwaalika watu. Basi hebu tupate changamoto ya kwenda barabarani na mipakani ili kuwashurutisha watu kuja. Kuna maelfu ya watu ambao wanahitaji uponyaji na neema ya wokovu wa Yesu Kristo. Hebu basi twenende na kuhubiri ujumbe mmoja zaidi, tufanye ombi moja zaidi, tufikie nafsi moja zaidi.

Mtu mmoja anapookoka utukufu wote unarudi kwake Mungu. Lakini ni furaha iliyoje sisi kuwa sehemu ndogo ya kazi hii kuu ya kiungu. Basi wewe mwenzangu unayeshiriki kazi hii ya injili endelea tu kuwaalika watu , kwa maana Mungu angali anaitana. ■